

## 7.JINSI YA KUVUNA NA KUHIFADHI

- Kunde zivunwe wakati zimekauka vizuri.Vuna kwa kuchuma vitumba au kung'oa mashina kama vitumba vyote vimekauka.
- Anika kunde zilizovunwa juani kisha piga na fito, peta anika juani zikauke vizuri kisha hifadhi ghalani. Kunde hubunguliwa haraka, kwahiylo hifadhi ndani ya mifuko maalaum (PICS bags).



**Kunde zilizohifadhiwa kwenye mifuko ya PICS**

## 8. KIASI CHA MAVUNO

Kunde za muda mrefu zinaweza wa kutoa magunia 6 hadi 8 kwa ekari moja au kilo moja,500-2,500 kwa hekta, na zile za muda mfupi magunia 6 hadi 7 kwa ekari au kilo 1,200 -2,000 kwa hekta kulingana na matunzo.



### **Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

1. Mkurugenzi wa Kanda,Utafiti na Maendeleo Kanda ya Mashariki, Kituo cha utafiti wa Kilimo, ILONGA, S.L.P 33, Kilosa,
2. Mkurugenzi wa Kanda, Utafiti na Maendeleo Kanda ya Kati, Kituo cha utafiti wa Kilimo, Makutupora, S.L.P 1676, Dodoma.
3. Afisa kilimo na Umwagiliaji, Halmashauri ya Wilaya Kongwa, S.L.P 57, Kongwa.

### **Kimetayarishwa na;**

Kituo cha utafiti wa kilimo, Ilonga , Sanduku la Posta 33, Kilosa, Morogoro, kikishirikiana na Taasisi ya utafiti wa kilimo ukanda wa tropiki (IITA), S.L.P. 34441, Dar Es Salaam,Tanzania, Kupitia mradi wa N2Africa



# **Lima kunde kwa lishe na kipato zaidi**



## KILIMO BORA CHA KUNDE

### 1. UTANGULIZI

Kunde ni zao jamii ya mikunde. Faida kubwa ya zao hili ni:

- Chanzo cha viini lishe vya protini kwa binadamu na wanyama.
- Mabaki ya mmea wa kunde ni chakula kizuri cha mifugo.
- Hurutubisha udongo.

### 2. AINA ZA KUNDE

#### Kunde za muda mrefu

- **Tumaini:** Hutambaa na kuchukua muda wa siku 75-85 kukomaa
- **Fahari :** Hutambaa na huchukua muda wa siku 90 kukomaa.
- **Raha-1 :** Haitambai na huchukua muda wa siku 74-80 kukomaa
- **Raha-2:** Haitambai na huchukua muda wa siku 70-75 kukomaa.

#### Kunde za muda mfupi

- **Vuli-1 :** Haitambai na huchukua siku 55-65 kukomaa.
- **Vuli-2 :** Haitambai na huchukua siku 65-70 kukomaa.

### 3. WAKATI WA KUPANDA

- Sehemu zenyе misimu miwili ya mvua, kunde za muda mrefu zipandwe wakati wa masika (miezi miwili na nusu kabla ya kumalizika mvua).
- Kunde za muda mfupi zipandwe wakati wa wavuli, ili kumwezesha mkulima kupanda zao la aina nyingine kama mtama, mahindi au pamba katika shamba hilo wakati wa masika.
- Sehemu zenyе msimu mmoja wa mvua kunde za muda mfupi zipandwe miezi miwili kabla ya kumalizika kwa mvua.

### 4. NAFASI YA KUPANDA

- Kunde zinazotambaa zipandwe kwenye nafasi ya sentimita 75 mstari hadi mstari na sentimita 20 shina hadi shina kwa kuweka mbegu mbili katika shimo. Wiki moja baada ya kuota punguza ubaki mche mmoja kila shimo.
- Kunde zisizotambaa zipandwe kwenye nafasi ya sentimita 50 mstari hadi mstari, na sentimita 20 shina hadi shina kwa kuweka mbegu tatu kila shimo. Wiki moja baada ya kuota punguzia ibaki miche miwili kila shimo.

### 5. PALIZI

Kwa matokeo mazuri, palilia kunde wiki 2 baada ya kupanda.

### 6. KUZUIA WADUDU

Ili kupata mavuno mengi kuzuia wadudu waharibifu kwa kupulizia dawa utakazo shauriwa na mtaalamu wa kilimo.

- Kwa kunde za muda mrefu, pulizia dawa mara tatu kuanzia wakati wa kutoa maua halafu kila bada ya siku kumi. Kwa kunde za muda mfupi, pulizia dawa mara mbili (baada ya kutoa maua na siku kumi baadaye).
- Kuna misimu ambapo wadudu wanaokula majani waitwao **Vifurunzi** au **Vikombe** hutokea kwa wingi. Wadudu hawa hutokea mara baada ya mimea kuota na wakitokea kwa wingi wanaweza kuleta hasara kubwa. Ili kuzuia wadudu hawa, weka dawa aina ya “**Marshal**” kwenye mbegu kabla yakupanda.



*Unyuniyiziaji wa dawa kuua wadudu wanaoshambulia kunde shambani*